

## Chuo cha MKU chatenga Sh1bn kwa kitengo cha uhandisi

**CHUO** Kikuu cha Mount Kenya kimetenga Sh1 bilioni za kujengea kitengo cha kufunza uhandisi, ili kuwa na wahandisi wenye ujuzi wa hali ya juu eneo la Afrika Mashariki na Kati.

Mwenyekiti wa chuo hicho, Prof Simon Gicharu, alisema kitengo hicho kitagharimu takribani Sh1 bilioni kwa minajili ya kupata wahandisi wenye ujuzi kamili wa kubuni mambo mapya. Alisema tayari chuo hicho kilipokea msaada wa Sh90 milioni, kutoka kwa shirika la *Africa Economic Reserch Consortium*, za kuwafadhili mahafala waliokamilisha masomo yao kwa lengo la kujisimamia kwa kubuni mambo mapya.

"Tungetaka kuona wanafunzi waki-jitegemea wanapokamilisha chuo," alisema Prof Gicharu.

Na Lawrence Ongaro